

Mapungufu ya Mpango wa Taifa wa Vocha za Pembejeo za Kilimo (NAIVs) ni yapi?

Mpango wa Taifa wa Vocha za Pembejeo za Kilimo (NAIVs) una lengo la kuongeza uzalishaji na uhakika wa chakula miongoni mwa wakulima wadogo. Hata hivyo, kuna matatizo mengi na changamoto za programu hii:

- ▶ Mpango umehamasisha utegemezi wa hali ya juu wa wakulima.
- ▶ Mavuno ya wakulima yameongezeka kwa karibu tani 2.5 milioni za mahindi na mpunga, lakini haijulikani kuwa ongezeko hili ni matokeo ya NAIVs au ni upanuzi wa kilimo cha mpunga au mahindi katika mashamba yao mapya – kwasababu matumizi ya pembejeo yamepungua hapa nchini.
- ▶ Takwimu za serikali kuhusu uzalishaji wa Mahindi siyo sahihi.
- ▶ Kwa kiasi kikubwa imenufaisha kaya zinazozalisha zaidi ambazo zinamudu kulipia asilimia 50 ya gawiwo la gharama za pembejeo za kilimo.

